Al-Islam.org
Ahlul Bayt Digital Islamic Library Project
Published on *Al-Islam.org* (https://www.al-islam.org)

Ushairi Wa Safiyyah Akiomboleza Kifo Cha Mtume [s]

Bibi Safiyyah binti Abdil-Muttalib (Shangazi ya Mtume) alisoma Qasida baada ya kufariki Mtume [s] kuomboleza kifo chake, na sehemu ya Qasida hiyo ni hii ifuatayo:

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu wewe ndiyo matumaini yetu, ulikuwa mwema wetu na wala hukuwa mnyanyasaji, na ulikuwa mwema mpole ewe Mtume wetu, basi leo na akulilie yeyote mwenye kulia."[1]

Katika kipande hiki cha shairi ambacho kilisomwa mbele ya masikio ya Masahaba, nao wanahistoria wakakisajili tunapata faida ya mambo mawili:

Kwanza: Kuzisemesha roho na hasa kumsemesha Mtume baada ya kufa ni jambo lililokuwa linafaa na likitumika tangu hapo mwanzo, na bibi Safiyyah anaposema: "Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu" kusema hivi haikuwa ni usemi wa kipuuzi na mchezo tu, au ni shirki kama wanavyodai Mawahabi wapotovu.

Pili: Bibi Safiyyah aliposema, "Wewe ndiyo matumaini yetu" inajulisha kwamba Bwana Mtume [s] ndiye matarajio na matumaini ya jamii ya Kiislamu katika nyakati zote na kila hali na wala hauwezi kukatika au kumalizika uhusiano wake na jamii hiyo hata baada ya kufariki kwake.

1. (1) Dhakhairul-uqbaa cha Al-hafidh Al-Muhibbu At-Tabari, uk. 252. (2) Maj-mauz-zawaid, juz. 9, uk. 36.

Source URL:
https://www.al-islam.org/uchunguzi-juu-ya-uwahhabi-ayatullah-jafar-subhani/ushairi-wa-safiyyah-akiomboleza-kifo-cha-mtume-s#comment-0